

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

**Simu:** +25526-230081  
**Nukushi:** +25526-2321170  
**Barua pepe:** [km@habari.go.tz](mailto:km@habari.go.tz)  
**Tovuti:** [www.habari.go.tz](http://www.habari.go.tz)



S. L. P 25,  
Mtaa wa Habari,  
Mji wa Serikali Mtumba,  
40481 Dodoma.

**TAARIFA KWA UMMA**

**KIKAO CHA KUKUSANYA MAONI YA KUBORESHA MPANGO MKAKATI WA  
TAIFA WA MAENDELEO YA MICHEZO**

**Dodoma- Desemba 17, 2020**

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Hassan Abbasi anawaalika wadau wa sekta ya michezo kwenye kikao cha kukusanya maoni kwa ajili ya kuandaa Mpango Mkakati wa Taifa wa maendeleo ya michezo.

Kikao hicho kitafanyika siku ya Jumamosi Desemba 19, 2020 kuazia saa tatu asubuhi (03:00 asubuhi) katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. Mgeni Rasmi atakuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa (Mb). Hivyo, uongozi wa wizara unawaomba viongozi wa vituo vya kulea vipaji vya michezo, maafisa michezo, viongozi wa vyama na mashirikisho pamoja na wadau malimbali walioalikwa kufika katika kikao hicho ili kutoa maoni ambayo yatasaidia kuboresha makakati wa maendeleo ya michezo nchini.

Aidha, Serikali inatambua na kuthamini umuhimu wa michezo kwa sababu ni nyenzo muhimu katika kuendeleza utamaduni katika jamii, kujenga afya, tabia ya ushirikiano na uzalendo.

Hivyo, utoaji wa maoni yenu yatakuwa ni mchango mkubwa katika kuboresha maendeleo ya michezo nchini.

Kwa mawasiliano zaidi piga simu Na. 0655242461 au 0767505313.

Imetolewa na;

Eleuteri E. Mangi

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**